



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3
Nukushi: +255 (0)22-2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796,
11992 - Dar es Salaam,
TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. NBS/N.20/2/105

Tarehe: 13 Agosti, 2015

TAARIFA KWA UMMA

PATO LA TAIFA ROBO YA KWANZA YA MWAKA (JANUARI – MACHI) 2015


Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina jukumu la kutayarisha na kusambaza takwimu rasmi nchini ikiwa ni pamoja na takwimu za Pato la Taifa kwa robo Mwaka. Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka hupimwa kwa kuangalia thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini katika vipindi vya miezi mitatu mitatu ambavyo ni Januari – Machi, Aprili – Juni, Julai – Septemba na Oktoba - Desemba. Utayarishaji wa takwimu za Pato la Taifa hujumuisha shughuli zote za kiuchumi na hivyo hutumika katika kutathmini, kupanga mipango na kutayarisha sera za kiuchumi.

Takwimu za robo mwaka ya kwanza zinazowasilishwa (Januari – Machi) kwa **bei za miaka inayohusika na mwaka wa 2007 zinasambazwa kwa mara ya kwanza** ambazo zimetayarishwa kwa kuzingatia marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007.

Matokeo ya takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka kwa bei za miaka inayohusika yameonyesha kuwa thamani ya Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ilikuwa TZS 21.9 trilioni ikilinganishwa na TZS 18.6 trilioni ya robo mwaka ya kwanza mwaka 2014.

Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza linaonyesha kuwa na jumla ya thamani ya TZS 10.6 trilioni kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na TZS 9.9 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2014, hii inamaanisha kuwa Pato la Taifa liliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.5 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 8.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Kielelezo 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo ya kwanza, Januari hadi Machi, 2006 – 2015



UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Ukuaji wa Sekta ya Kilimo na Mifugo

Shughuli za kiuchumi za kilimo na mifugo zilikuwa kwa kasi ya asilimia 2.6 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 3.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2014

Katika kipindi husika, kilimo cha **Mazao** kilikuwa kwa asilimia 2.7 kwa robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 4.3 kipindi kama hicho mwaka 2014; Ukuaji wa shughuli za **Ufugaji** uliongezeka kwa asilimia 2.9 robo ya kwanza mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 2.2 kipindi kama hicho mwaka 2014; ukuaji wa shughuli za **Misitu** uliongezeka kwa asilimia 2.1 kwa robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 5.0 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Uvuvi** ziliongezeka kwa asilimia 0.9 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 2.3 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Ukuaji sekta ya kilimo na mifugo ulitokana na jitihada za serikali kuwasaidia wakulima kwa kutoa ruzuku na maelekezo ya ma-ofisa Ugani kwa wakulima kama vile kuchagua mbegu bora yalisaidia kuongeza uzalishaji.

Shughuli za Uchumi za Viwanda na Ujenzi

Shughuli za **Uchimbaji Madini, Mawe na Kokoto** ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 0.6 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 19.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Uzalishaji wa dhahabu katika kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka 2015 ulikuwa kg 10,458 ikilinganishwa na kg 10,711 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Uzalishaji wa Almasi katika kipindi cha robo ya kwanza 2015 ulikuwa karati 72,086 ikilinganishwa na karati 94,278 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Madini ya Tanzanite yaliyozalishwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 yalikuwa kg 1,606 ikilinganishwa na kg 4,118 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Uzalishaji bidhaa Viwandani** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 5.7 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 8.2 kipindi kama hicho mwaka mwaka 2014. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za vyakula, vinywaji, tumbaku, nguo, simenti na bidhaa za kemikali na madawa.

Shughuli za **Uzalishaji nishati ya umeme na maji** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 10.7 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Kuongezeka kwa ukuaji wa nishati ya umeme kulitokana na kuongezeka kwa umeme uliozalishwa kutoka kwenye mitambo inayotumia, maji, mafuta na gesi asilia.

Kwa upande mwingine shughuli za uzalishaji wa nishati ya umeme zilikuwa kwa asilimia 13.0 kwa robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 18.1 kwa robo mwaka ya kwanza ya mwaka 2014.

Shughuli za **Ujenzi** (ambazo zinajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi na zisizo za makazi; barabara na madaraja; na shughuli nyingine za uhandisi) katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 zilikuwa kwa asilimia 8.8 ikilinganishwa na asilimia 21.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Ukuaji wa Shughuli za Uchumi za Utoaji Huduma

Shughuli za **Biashara za jumla na reja reja, Ukarabati wa Magari na Pikipiki na Vifaa vingine vya Nyumbani** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 6.5 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Uchukuzi na Uhifadhi** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 12.9 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 14.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli nyingine kama vile huduma za **Malazi na Chakula** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 1.7 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 3.4 kipindi kama hicho 2014, shughuli za **Habari na Mawasiliano** zilikuwa kwa asilimia 10.3 katika robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 17.1 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Fedha na Bima** katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2015 ziliongezeka kwa asilimia 9.1 ikilinganishwa na asilimia 11.2 kipindi kama hicho mwaka 2014. **Upangishaji nyumba** ulikuwa kwa asilimia 2.2 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 2.1 kipindi kama hicho mwaka 2014, **Huduma za kitaalaamu; Kisayansi na Ufundi; Utawala na huduma nyinginezo** zilikuwa kwa asilimia asilimia 8.6 robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 8.2 ya kipindi kama hicho mwaka 2014.

Aidha, Shughuli za **Uendeshaji Serikali** zilikuwa kwa asilimia 12.0 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.2 kipindi kama hicho mwaka 2014. Huduma za **Elimu** zilikuwa kwa asilimia 6.7 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2014, huduma za **Afya** zilikuwa kwa asilimia 8.0 kwa robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 8.4 kipindi kama hicho 2014 na shughuli za **Sanaa na Michezo** zilikuwa kwa asilimia 5.6 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 7.2 kipindi kama hicho mwaka 2014, **Huduma nyinginezo** zilikuwa kwa asilimia 6.8 kwa robo mwaka ya kwanza 2015 ikilinganishwa na asilimia 6.6 ya kipindi kama hicho mwaka 2014 na shughuli nyingine za **Kaya zinazoajiri** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 2.6 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2015 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 2.7 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Kwa mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu,

Ofisi ya Taifa ya Takwimu,

Dar es Salaam.